II. Mkutano wenyewe. Shughuli za mkutano *huongozwa na mwenyekiti*, ambaye katika *kamati ya kawaida huchaguliwa* kati ya wanachama walioko. Inapotokea *kamati mahsusi*, mwenyekiti anaweza *kuteuliwa wakati kamati hiyo inapoundwa* na kuambiwa *masharti yake*. *Makamu wa mwenyekiti pia huteuliwa au huchaguliwa na wakati mwenyekiti wa kawaida hayopo atakuwa naibu wa mwenyekiti*. *Anayeshikilia kiti namna hii* (yaani *mwenyekiti wa muda*) ana uwezo na haki sawa na mwenyekiti wa kawaida, pamoja na kuwa na haki ya *kura ya uamuzi*. Hii ni kura ya pili ambayo mwenyekiti anaweza kuitumia ikiwa kumetokea *usawa wa kura*. (Kwa Kiingereza kura yake ya kwanza au kura yake ya kawaida mara nyingine huitwa "deliberative vote", lakini neno hili "deliberative" halina maana yoyote maalumu.)

Dondoo la kwanza katika *ajenda huwa lina kichwa "kuthibitishwa kwa kumbukumbu za mkutano"*; chini ya kichwa hiki, wanachama husoma kumbukumbu za mkutano uliopita (ijapokuwa huchukuliwa "*kama kwamba zimesomwa*" ili kuhifadhi wakati) na *kuthibitisha kwamba ni sawasawa na mwenyekiti baadaye huzitia sahihi*. Hili likishafanyika, wanachama wanaweza kujadili *mambo yoyote yanayotokana na kumbukumbu*; kwa mfano, ikiwa katika kumbukumbu *kumeandikwa uamuzi kwamba katibu achunguze jambo fulani na atoe taarifa juu yake katika mkutano ufuatao*, anaweza sasa

akaombwa kutoa *taarifa ya mdomo* juu ya uchunguzi wake. Kumbukumbu zenyewe ni *kumbukumbu za kudumu zilizoandikwa* kuhusu mambo *yaliyofanywa* katika mkutano, na ni kazi ya katibu *kuweka kumbukumbu hizi*. Baadhi ya kamati rasmi, kama vile za Bunge au za konseli ya mitaa, huanza mikutano yao kwa dua. Mtu mmoja (kwa kawaida mwenyekiti, lakini kasisi au kadhi, n.k., akiwepo mmojawapo *anayetumikia kamati*) anaweza *kusoma* dua, au mkutano unaweza *kufunguliwa kwa dua ya kimya*. Hili huandikwa kuwa ni kumbukumbu ya kwanza.

Kabla ya mkutano kuweza *kufanya shughuli yoyote kirasmi au kisheria*, ni lazima kuwepo na *kiwango* cha wanachama, yaani idadi maalumu ya wanachama ni lazima wawe wamehudhuria. Idadi hii maalumu ya wanachama husemekana kuwa *wamekamilisha kiwango*, na iwapo wakati wowote mmojawapo wa wanachama *anamtanabahisha mwenyekiti* kwamba wale waliohudhuria wamepungua idadi hiyo, ni lazima *asimamisha kikao* mpaka waweko (wanachama) wa kutosha wa kukamilisha kiwango. Ikiwa mwanachama yeyote mwingine hakutokea ni lazima *auahirishe* mkutano mpaka siku nyingine, au anaweza kuuahirisha *bila ya kuchagua siku maalumu (sine die—yaani bila ya kutaja siku ya kuyarudia majadiliano)*. Itokeapo hivi, kamati *itakutanika* tena siku yoyote ifaayo wakati ujao.

Baada ya dua na *kuthibitishwa kwa kumbukumbu*, mwenyekiti ana haki ya kutoa *tamko*; tamko hilo huitwa *hotuba ya mwenyekiti* au *taarifa ya mwenyekiti*. *Wanachama wa kawaida* (au *wanachama halisi*) wa kamati kwa kawaida huweza kujadili taarifa ya mwenyekiti, lakini yeyote *“aliyekuwepo”* (yaani si mwanachama halisi lakini alialikwa na kuwa mgeni au *anayekuwepo* ili atoe mashauri, kama vile maafisa wakuu wa halmashauri) hawawezi *kushiriki* katika majadiliano au katika *upigaji kura*. Hata ikiwa mwenyekiti hatatoa taarifa, kwa kawaida atasema maneno machache ya kuanzisha shughuli za mkutano na haya huitwa *maneno ya utangulizi*. (Kumbuka kuwa tunasema kuwa wanachama halisi “huhudhuria” katika mkutano, lakini wasiokuwa wanachama “huwepo” mkutanoni.)

Madondoo mengine katika ajenda hushughulikiwa moja moja, kwa kawaida kwa utaratibu wa jinsi yalivyopangwa. *Maamuzi* yote ya kamati ni lazima yafanywe kwa kupigia kura *hoja*. Mwenyekiti akiona kwamba maongezi (au majadiliano) juu ya jambo maalumu yameendelea kwa muda mrefu *huitisha hoja itolewe*; hoja hii ni *azimio* lililopendekezwa kiada na mwanachama ambaye anaitwa *mwazimu* wa hoja au *mtoa hoja*. Baada ya hoja *kutolewa* au *kuazimiwa*, mwenyekiti *hutafuta mwafiki*, kwa sababu katika kamati zote mwanachama mwingine ni lazima *aunge mkono* hoja kiada, kabla ya mwenyekiti *kuamuru ipigiwe kura*; jambo hili huitwa *kua-fiki hoja*, na mwanachama afanyaye hivyo huitwa *mwafiki*. Baadaye wanachama *hupiga kura* (kwa kusema “ndiyo” ikiwa *wanaipendelea* hoja hiyo, au “siyo” ikiwa *wanaipinga*, lakini upigaji kura unaweza kufanyika *kwa kuinua mkono* au hata *kwa siri*, ambapo kila mwanachama huandika “ndiyo” au “siyo” katika kijikaratasi, bila ya kuandika jina lake). Idadi ya wale wa-

naopigia kura hoja na wale *wanaoipinga* hoja huhesabiwa na mwenyekiti na kwa kawaida na katibu ambaye pia *huandika* hoja hiyo *neni kwa neno*. (Ni muhimu sana kuwa kumbukumbu ya hoja iandikwe neno kwa neno; katibu hana ruhusa kabisa kubadilisha *mpango wa maneno*.) Ikiwa *wengi wa wanachama* wamepiga kura kuunga mkono hoja husemekana kuwa hoja hiyo *imepitishwa* na baadaye huwa ni “*uamuzi*” wa kamati. Kupitisha hoja, kwa hivyo, kuna maana kuwa kamati *inathibitisha azimio* na *kulikubali* litekelezwe. Iwapo wengi wataipinga hoja hii husemekana kuwa “*imekataliwa*”. (Kwa Kiingereza maneno haya “*carried*” na “*lost*” hutumiwa pia kwa maana ya “*kupitishwa*” na “*kukataliwa*” hoja.) Ikiwa hoja imekataliwa, hapana mwanachama anayeweza *kulirudia jambo* lile katika mkutano huo. Kwa hivyo, kazi kubwa ya kamati si majadiliano, kama wanavyodhani watu wengi, lakini ni *kupitisha maamuzi*. *Uamuzi wa wingi* ni uamuzi wa mwisho, ijapokuwa wingi huo ni mdogo sana (ingawa katika nyakati nyingine kanuni za kamati huenda zikataja kuwa baadhi ya maazimio yanaweza tu kupitishwa *na wingi wa thuluthi mbili* au kiwango kingine kinachojulikana wazi).

Wanachama wote wanaweza *kuisemea* hoja yoyote; wanaweza *kusema* (*kuijadili*) *kwa kuiunga mkono* (yaani, wanaweza kuizungumza ili *kuliridhia azimio la mtoa hoja*) au kuonyesha *ukinzani wao juu yake* (yaani *kui-pinga*), lakini mtoa hoja anatazamiwa wakati wote *kuiunga mkono azimio lake*.

Mwanachama hana lazima ya *kupiga kura*; akipenda anaweza *kujitenga* (yaani kutopiga kura). Pia, baada ya mwanachama *kutoa hoja*, majadiliano huenda yakamfanya mtoa hoja mwenyewe akaamini kuwa hoja hiyo si nzuri, na wakati huo akaomba *iondoshwe*. Fahamu kuwa kanuni za nidhamu hazimruhusu kabisa mwanachama kudokeza *upinzani wake juu ya hoja* isipokuwa kwa njia ya *kusema kwa kuipinga waziwazi* (au kinaganaga) *wakati wa majadiliano*.

Baada ya shughuli zote za ajenda kumalizika kwa kufuatia nidhamu hii (zikiwamo “shughuli nyingine zozote”), mwenyekiti *huufunga* mkutano kiada kwa kusema “Natangaza kufungwa kwa mkutano”.

Mwenyekiti ni lazima pia kusimamia *mwenendo* wa wanachama katika mkutano. Wakivunja kanuni za majadiliano hulazimika *kuwakumbusha nidhamu*; iwapo wanachama wengi wanazivunja kanuni (k.m. kwa kupiga sogu au kwa kufanya fujo mtu mwingine anapozungumza), husemekana kuweco kwa “*mwenendo wa fujo*”, na ni lazima kwa mwenyekiti *kuwaku-mbusha wanachama nidhamu ya mkutano*. Ikiwa mwanachama amefanya kosa la *kuwa na mwenendo mbaya sana* au *mwenendo mbaya* wa mfululizo wakati wa majadiliano, mwenyekiti anaweza kumwomba *aombe radhi* (au *msamaha*), na iwapo atakataa kufanya hivyo, mwenyekiti anaweza kumwamrisha kuondoka mkutanoni. Kitendo hiki huitwa *kumsimamisha kazi mwanachama*. Kanuni moja iliyo muhimu ni kwamba wanachama hawana ruhusa ya *kukatiza* wakati mtu mwingine anapozungumza (yaani mwingine

anapopewa uwanja), ingawa mwanachama yeyote anaweza kujitia kati *kumtanabahisha mwenyekiti kwamba* huyo anayesema anavunja baadhi ya kanuni za kamati. Kwa ajili ya jambo hili, kwa kawaida mwanachama huihua mkono wake na kusema “Bwana Mwenyekiti, nidhamu”; katika mkutano rasmi wa hadhara ni lazima asimame mpaka mwenyekiti atakapomwona na kisha aseme “*Nimesimama, Bwana Mwenyekiti, kwa ajili ya nidhamu*”. Hapo mwenyekiti atamwomba mwanachama anayezungumza kukaa hadi wakati ambapo atakuwa amekwisha zingatia hiyo nidhamu; baada ya kuzingatia hutoa *uamuzi* wake; ama huamua kwamba *mwanachama anavyosema ni sawa* au kuamua kwamba *anavyosema mwanachama si sawa*. Atasema “Naamua asemavyo mwanachama ni sawa (au si sawa) kwa sababu . . .” na kisha atoe maelezo mafupi juu ya uamuzi wake. Iwapo mwanachama atatoa dai au shtaka kali, anaweza akaombwa *alithibitisha*, yaani mwenyekiti anaweza akashikilia kwamba atoe sababu ya kutosheleza iliyomfanya aseme hili alilolisema (hana lazima ya kuthibitisha kwamba shtaka hilo ni la kweli—bali kuwa alikuwa na sababu ya kutosha kuamini kuwa lilikuwa ni kweli wakati alipolitamka).

III. Sehemu ya tatu ya nidhamu ya kamati huanza baada ya mkutano kufungwa. Sehemu hii ni ya uandikaji kumbukumbu. Wakati wa mkutano, katibu huandika maelezo kamili *kwa ajili ya kuweka kumbukumbu*, kwa kuwa ni muhimu kwamba shughuli zote za kamati ni lazima *ziwekwe katika kumbukumbu*, iwapo mashaka au upinzani huenda ukatokea baadaye. Hata hivyo, katibu si lazima kuandika maelezo ya majadiliano yote au maneno yote yaliyotolewa au maoni yote yaliyotolewa; yeye huandika *juu ya yale yaliyofanywa*. Katika kumbukumbu katibu kwanza huandika majina ya wale *WALIOHUDHURIA*. Kisha huandika majina ya wale waliotaka radhi kwa *kutohudhuria*, na kuanza kuandika maneno “Wasihudhuria na kutaka radhi” (au “Barua za kuomba radhi ya kutohudhuria zilipokewa kutoka kwa Mabwana . . .”). Kisha huendelea na orodha ya wale wasiokuwa wanachama, wageni n.k. kwa kutumia anwani hii: *WALIOKUWEPO*. Husajili kila dondo liliushughulikiwa katika *fungu* au *fasili* mbali; kila sehemu au fasili inaitwa *kumbukumbu* na huwa na anwani mkono wa kushoto wa ukurasa *KUMBUKUMBU NAMBA* . . . Baadhi ya makatibu wa kamati huandika jina la mtu anayependekeza hoja na yule mwenye kuafiki na pia iwapo hoja ilipitishwa *kwa (kura ya) pamoja* au *kwa wingi wa kura kadha wa kadha*, lakini kwa kawaida ni bora *kuacha* ukamilifu wa maelezo ya aina hii. Ikiwa mtu yeyote *amependekeza mabadilisho katika hoja* (kwa mfano, *kubadilisha* hoja kwa *kuacha* au *kuondosha* (au *kufuta*) baadhi ya maneno au kwa *kupenyeza* au *kuongeza* mengine, au *kugeuza* mengine badala ya yale yaliyopendekezwa na yule mtoa hoja), upigaji kura juu ya badilisho *hufanywa* kwanza na matokeo ya uchaguzi huu huingizwa kwanza katika kumbukumbu. Hoja ya kwanza (au ya asili) huitwa *hoja ya kiini*, kuitofautisha na hoja nyingine zinazotokana nayo, kama vile mabadilisho au *hoja ya kuahirisha* upigaji kura hadi wakati ujao.

Kumbukumbu huwa namna hii:

KUMBUKUMBU NAMBA 23/74: UTENGEZAJI WA KUMBI LA JAMII

Baada ya kuwepo majadiliano marefu (au baada ya majadiliano makali, n.k.), wakati ambapo wanachama kadha wa kadha wali-laumu hali ya sasa ya mali ya Konseli

ILIAMULIWA

Kwamba idadi ya shilingi 1,500/- zitengwe kwa ajili ya kutengeneza Kumbi la Jamii, pamoja na kupaka rangi upya milango na madirisha.

(Wakati kura ilipokuwa ikifanywa Bw Fulani aliingia mkutanoni na baadaye akamwomba mwenyekiti amwie radhi kwa kuchelewa.)

MAMBO MENGINE

Wakati mwingine watu wenye vyeo maalumu huwa siku zote ni wanachama wa kamati kwa sababu ya vyeo vyao, si kwa sababu wao ni watu waliochaguliwa kwa kupigiwa kura (k.m. Mkuu wa Wilaya siku zote anakua ni mwanachama wa Kamati ya Maendeleo). Hali kama hii ikitokea, mwanachama huyu huitwa *mwanachama kwa cheo*.

Katika mkutano hadhara watu wanaweza kuonyesha kuridhika au kutoridhika kwa wale wanaowawakilisha au kwa afisa yeyote mwingine (k.m. mwenyekiti, katibu, *mweka hazina*, n.k.) kwa kupitisha hoja. Wanaweza kuonyesha hali yao ya kumwunga mkono mwenyekiti, kwa mfano, kwa kupitisha kura ya kuwa na imani juu yake, au kuonyesha kupinga kwao kwa kupitisha kura ya kutokuwa na imani, au hata kupiga kura ya kulaumu (ambayo inadokeza kuwa wanapinga tabia yake au vitendo vyake vikali). Pia wanaweza kupitisha hoja maalumu ya shukrani kwa mtu fulani kwa ajili ya shughuli maalumu. Hizi ni hoja za kawaida na hupitishwa kwa kufuata nidhamu ya kawaida, ingawa shukrani mara nyingi hupitishwa bila ya kuwako majadiliano.

Mara nyingine mwenyekiti anaweza kwamua kwamba jambo fulani lichukuliwe kama kwamba limekwisha katiwa shauri au kufanyika bila ya mwenyekiti kuamuru kura, lakini jambo kama hili si la kawaida katika kamati za kawaida (ingawa hutokea mara kwa mara katika Bunge).

Kamati inaweza ikazingatia jambo ambalo halihitaji uamuzi, na katibu mara nyingi atalisajili jambo kama hilo katika kumbukumbu kwa kuandika "Kamati ilitambua kwa shukrani (au kwa masikitiko, kwa furaha, kwa kupendezwa, kwa *mashaka*, n.k.) kwamba..."

Kamati mahsusi inapomaliza kufanya shughuli, ambayo kwayo iliundwa, mwenyekiti (au mkutano wa kamati kuu) anaweza *kuivunja kamati hiyo*, na kutoka wakati huo huwa haiko tena.

Kamati inaweza *ikageza* uamuzi juu ya moja ya maamuzi yake; ili ifanye hivi ni lazima ipitishwe hoja maalumu *kutangua* ule wa mwanzo. Fahamu kuwa *utanguzi* wa hoja unahitaji hoja nyingine kutolewa katika mkutano mwingine ujao.

Iwapo mwanachama au jamii yake itaifaidika kwa uamuzi fulani, mwanachama huyu hana ruhusa ya kushiriki katika majadiliano au katika upigaji kura juu yake. Badala yake itambidi *aaridhie masilahi yake ya binafsi*, aidha ama atoke chumbani au anyamaze kimya (kwa kulingana na uamuzi wa mwenyekiti) mpaka baada ya upigaji kura kumalizika. Lakini iwapo mwanachama anadhani kuwa matamshi au mwenendo au mawazo yake haya-kufahamika vyema, anaweza kuomba ruhusa ya *kutoa maelezo binafsi*, yaani *kujieleza*.

Kamati inaweza *kujaza* nafasi ya kiti kilicho wazi kwa *kumteua* mtu ambaye *angestahiki* kuchaguliwa katika hali ya kawaida. Huenda kukawa na *wateule* kadha wa kadha na hapo tena kamati ikapiga kura *kukubali au kupinga teuzi mbalimbali* kwa kupitia njia ya kawaida. Haifai kumchagua mtu ambaye *hatastahiki* kuteuliwa katika uchaguzi wa kawaida. Mara nyingine kamati huenda ikapewa uwezo wa *kuongeza* mwanachama mmoja zaidi; *kuongezwa* kwa mwanachama hufanywa kwa (kulingana na) *kura ya wingi* na kwa kufuata nidhamu ya kawaida, na *mwanachama wa kuongezwa* kwa kawaida anazo haki kamili za kupiga kura. Sharti ya *kustahili* au *kutostahili kuchaguliwa* ni lazima zielezwe katika *katiba ya kamati* au *masharti yaliyowekwa* au *yaliyokubaliwa*.

Kamati inaweza kuteua kamati nyingine kutokana na wanachama wake kwa ajili ya shughuli maalumu; kikundi hiki kidogo kinaitwa *kamati ndogo*. Kamati ndogo ambayo wanachama wake waliteuliwa kwa njia hii, mara nyingi huitwa *kamati teule*, hasa ikiwa imeteuliwa na Bunge. Kamati ambayo haivunjwi kamwe (ingawa wanachama wake wanaweza wakabadilishwa) inaitwa *kamati ya kudumu* (k.m. *kamati ya afya* au *kamati ya fedha* ya konseli). Kamati inapotaka kamati ndogo kuzingatia jambo, jambo hilo *hupelekwa* katika kamati ndogo. *Upelekaji* wa aina hii juu ya jambo hufanywa pia kwa kupitisha *hoja ya kiada*. Kamati ndogo kwa kawaida ina uwezo wa *kupendekeza* (au *kufanya mapendekezo*) tu. Uamuzi wa mwisho hufanywa na *kamati nzima*. Kamati nzima inapokata shauri kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati ndogo inasemekana kuwa *imekubali* taarifa ya kamati ndogo.

Wakati mwenyekiti anapoanzisha jambo au kueleza jambo lolote la shughuli (ya mkutano), wanachama hawawezi kumkatiza. Anapomaliza na wakati kuwadia kwa wengine kuzungumza, tunasema kuwa *anawapa wanachama uwanja*. Anaweza kusema "Sasa jambo lijadiliwe" au "Sasa wanachama wamepewa uwanja"

Wakati mwingine swali huulizwa katika mkutano wa kamati na majibu (kwa kuwa majibu hayakutosheleza au hayakukamilika au hudokeza juu ya jambo jingine linalosibu) yakahitaji swali jingine; hili linajulikana kwa jina la *swali la nyongeza*. (Bungeni, lazima kutolewe arifa iliyoandikwa (au arifa ya maandishi) kabla ya maswali ya aina fulani kuulizwa lakini swali la nyongeza kwa kawaida linaweza kuulizwa *bila ya arifa*.)

Katika hali fulani, wale wenye vyeo (katika chama cha ushirika, k.m.) huenda wakapewa ruhusa ya kuchukua hatua (ifaayo) bila ya kushauriana na kamati. Katika hali zote za aina hii ni lazima waandike taarifa na kuipeleka katika kamati baadaye na iwapo kamati itatosheka na hatua yao, *huthibitisha* uamuzi wao. *Kuthibitishwa* huku kwa hatua iliyokwisha chukuliwa kwa mara nyingi ni muhimu sana.

Ikiwa mkutano umeitishwa lakini hauwezi kufanywa katika wakati ule ulioarifiwa, husemekana kuwa *umekawilishwa* (tazama tofauti kati ya *kukawilishwa* kwa mkutano na *kuahirishwa* baada ya kuanzishwa).

Neno hili "honorary" kwa Kiingereza linalotumiwa katika kamati lina maana ya "bila ya malipo" na kwa Kiswahili hutaja "*Mweka Hazina Asiye-lipwa*" (Hon. Treasurer) au "kazi isiyolipiwa", "cheo kisicholipiwa" (an honorary post), n.k.

Mwisho kabisa, kamati ni lazima *kupanga maneno* ya maamuzi kwa hadhari kubwa; mambo muhimu ya kisheria mara nyingi hutegemea ule *mpango halisi wa maneno* uliotumiwa.

Appendix "B" to First List of Recommended Terms for Committee Work

Committee Work and its Technical Terms

All committees should follow a *standard procedure*; that is, a procedure that has been authorized or that has grown up by custom and has been found useful. When all the *rules* of procedure are followed strictly, we speak of *formal procedure*; when some of the less important rules are *waived* we speak of *informal procedure*. The main parts of standard procedure are as follows.

I. A meeting is *convened* (by the *chairman*) and an *agenda paper* drafted and *circulated* to the *members* (usually by the *committee clerk* or *secretary*). The chairman usually tells the members about a meeting by *giving written notice*, but in the case of an *urgent meeting* he may give *verbal notice* instead. Each section of the agenda represents one *matter* that is to be *discussed* at the meeting; that is, one *item* of the *business* that the committee is to deal with. Usually, the last *heading* is "*any other business*" (abbreviated to A.O.B.), and when the meeting reaches this stage any member can raise any point that he would like discussed.

II. The meeting itself. The business of a meeting is *conducted* by the chairman, who in the case of an *ordinary committee* is usually *elected* from among the members. In the case of a *special* or *ad hoc committee* the chairman may be appointed at the time when the committee is *set up* and given its *terms of reference*. A *vice-chairman* also is usually appointed or elected, and *in the absence* of the regular chairman he will act as *deputy chairman*. Such an *acting chairman* (that is, a *temporary chairman*) has exactly the same powers and rights as a regular chairman, including the right to a *casting vote*. This is a second vote that a chairman can cast if there is a *tie* in the *voting*. (In English his first or ordinary vote is sometimes called his "deliberative vote", but the word "deliberative" really has no special meaning.)

The first *item* on the *agenda* usually has the heading "*confirmation of minutes*"; under this heading the meeting reads the minutes of the previous meeting (though they are usually "*taken as read*" to save time) and *confirms* that they are correct, and the chairman then *signs* them. When this has been done the meeting can discuss any *matters arising from the minutes*; for example, if the minutes record a *decision* that the secretary should investigate something and *report* on it at the next meeting, he can now be asked to give a *verbal report* on his investigation. The minutes themselves are a *permanent record in writing* of the proceedings at a meeting, and it is the secretary's job to *keep* this record. Some very official com-

mittees, such as Parliament or a local council, open their meetings with *prayers*. Someone (normally the chairman, but a clergyman or kadhi, etc.. if there is one *servng* on the committee) may *read a prayer*, or the meeting may *open with silent prayers*. This is recorded as the first minute.

Before a meeting can *transact* any business officially and legally, there must be a *quorum* of members; that is, a certain number of members must *be present*. This fixed number of members is said to *constitute a quorum*, and if at any time someone *calls the chairman's attention to the fact that* those who are present are less than this number, he must *suspend the sitting* until there are enough to constitute a quorum. If no-one else comes, he must *adjourn* the meeting until another day, or he may adjourn it *sine die*; that is, without fixing a definite day to *resume the debate*. In that case the committee will *convene* again on some suitable day in the future.

After prayers and the *confirmation of the minutes*, the chairman has the right to make a *statement*; this is known as *the chairman's speech*, or as a *communication from the chair*. The *regular members* (or *full members*) of the committee can usually discuss the chairman's speech, but anyone who is "*in attendance*" (that is, who is not a full member but has been invited as a guest, or who *attends* in order to give advice when asked, such as the Chief Officers of a council) cannot *participate* in the debate or in any *voting*. Even if he does not give any special communication from the chair, the chairman will usually say a few words to introduce the business of the meeting, and these are known as his *preliminary remarks*. (Notice that we say that full members *are present* at a meeting, but that non-members *attend* it.)

The other items on the agenda are dealt with one by one, usually in the order in which they are arranged on the paper. All *decisions* of a committee must be made by means of voting on a *motion*. When he thinks that the discussion of an item has gone on long enough, the chairman *calls for a motion*; this motion is a *proposal put forward formally* (that is moved by some member, who is known as the *proposer* of the motion or the *mover* of the motion. After the motion has been *proposed* the chairman *calls for a seconder*, because in all committees some other member must *support* a motion formally before the chairman *puts it to the vote*; this is known as *seconding the motion*, and the member who does this is called the *seconder*. The members then *vote* (usually by saying "Ay" if they are *in favour* of the motion, or "No" if they *are against* it, but a vote can also be taken by a *show of hands*, or even by a *secret ballot*, where each member writes "Ay" or "No" on a piece of paper with no name on it). The total number of those who *vote for* a motion and of those who *vote against* it is counted by the chairman, and usually by the secretary as well, who also *makes a verbatim* record of the *wording* of the motion. (It is very important that this record of the motion should be verbatim; he must not change the wording at all.) If the *majority* of the members vote in favour of the motion it is said to be "*passed*", and it then becomes a "*resolution*" of the committee.

To pass a motion, therefore, means that the committee *approves* the *proposal* in it and *adopts* it to be carried out. If the majority votes against it, it is said to be "*rejected*". (In English the words "carried" and "lost" are also used for "passing" and "rejecting" a motion.) If a motion is rejected, no member can *raise the matter again* at that meeting. Thus, the main work of a committee is not discussion, as many people think, but *passing resolutions*. A *majority decision* is final, even though the majority is very small (though in some cases the rules of a committee may state that certain kinds of resolution can only be passed *by a two-thirds majority*, or some other definite proportion).

All members have a right to *speak* to any motion; they can *speak in support of it* (that is, they can speak in order to *endorse* the *mover's proposal*) or to express their *objections* to it (that is, to *oppose* it), but the mover of the motion is always expected to *speak in support of his own proposal*.

A member does not have to *cast a vote*; if he wishes he can *abstain*. Also, after a member has *moved a motion*, the discussion may convince the mover himself that it was not a good one, and he may then ask permission to *withdraw* it. Notice that the rules of procedure do not allow a member to indicate his *opposition to a motion* in any way except by *speaking against it openly during the debate*.

When all the business on the agenda has been dealt with according to this procedure (including "any other business"), the chairman formally *closes* the meeting by saying "I now declare the meeting closed".

The chairman must also control the *conduct* of members during a meeting. If they break the rules of debate he must *call them to order*; if many members are breaking the rules (for example by talking or making a noise while someone is speaking) we speak of "*disorderly conduct*", and the chairman must *call the meeting to order*. If a member is guilty of *grossly disorderly conduct* or persistent *misconduct* during a debate the chairman may ask him to *apologize*, and if he refuses the chairman may order him to leave the meeting. This is called *suspending the member*. One important rule is that members must not *interrupt* while another is speaking (that is, while the other "*has the floor*"), although any member may interject to *call the chairman's attention to the fact* that the speaker is breaking some rule of the committee. To do this, he usually raises his hand and says "Point of order, Mr. Chairman"; at a formal public meeting he should stand up until the chairman notices him and then say "*I rise on a point of order, Mr. Chairman*". The chairman then asks the member speaking to sit down until he has considered the point of order that has been raised; when he has considered it he gives his *ruling*; he either *rules the speaker in order* or *rules him out of order*. He will say "I rule the member in order (or: out of order) because . . ." and then gives a short explanation of his ruling. If a member makes any serious claim or charge, he may be asked to *substantiate* it; that is, the chairman may insist that he produces a good reason for saying what he did (he does not have to prove that the charge was actually true —only that he had real reason for thinking it was true when he made it).

III. The third part of committee procedure begins after the meeting has been closed. This is the writing of the minutes. During the meeting, the secretary makes detailed notes *for record purposes*, because it is important that all the transactions of the committee should be *on record* in case doubts or arguments should arise later. However, the secretary should not record all the debate or all the *remarks* made or all the opinions expressed; he records *what was done*. In the minutes the secretary *enters* first the names of *those who were present*, with the heading *PRESENT*. Then he enters the names of those who sent *apologies for being absent*, beginning with the words "*Apologies for absence were received from . . .*". Then he adds a list of non-members (guests, etc.) with the heading *IN ATTENDANCE*. He records each item of business in a separate *section or paragraph*, and each of these sections or paragraphs is itself called a minute and has a heading on the left side of the page: *MINUTE NO . . .* Some committee secretaries record the names of the mover and the seconder of each motion, and also whether the motion was passed *unanimously* or *by a majority of x votes*, but it is usually better to *omit* such details. If anyone has *moved an amendment* to a motion (for example, to *amend* the motion by *omitting* or *deleting* some words, or by *inserting* or *adding* others, or by *substituting* different words for the ones proposed by the mover), the vote on the amendment is *held* first and the result of this vote is entered first in the minutes. The original motion, by the way, is called a *substantive motion*, to distinguish it from other motions that arise from it, such as amendments or a motion to *defer* voting on it until later.

A minute looks like this:

MINUTE No. 23/74: *REPAIRS TO SOCIAL HALL*

After lengthy discussion (or: after heated discussion), during which several members criticized the present condition of the Council's property, it was

RESOLVED

That a sum of Sh. 1,500/- should be set aside for repairs to the Social Hall, including the repainting of the doors and windows.

(While the vote was being taken, Mr X entered the meeting and afterwards apologized to the Chair for his late arrival.)

OTHER POINTS

In some cases the holder of a certain job is always a member of a committee, because of his official position, not because he is elected as a person

(e.g., whoever is the D.C. in a district is always a member of the local Development Committee). In such a case he is said to be an *ex-officio* member.

A meeting can show its approval or disapproval of its representatives or of any office bearer (e.g., the chairman, the secretary, *the treasurer*, etc.) by passing special motions. They can show their approval of the chairman, for example, by passing a *vote of confidence* in him, or show their disapproval by passing a *vote of no confidence*, or even a *vote of censure* (which indicates that they disapprove of his conduct or actions very strongly). They can also pass a special *vote of thanks* to someone for some special service. These are ordinary formal motions and are moved and voted on in the ordinary way, though a vote of thanks is often passed *without debate*.

In certain circumstances the chairman may rule that something should be regarded as decided or done *without question put*, but this is unusual in ordinary committees (though it is common in Parliament).

A committee may consider something that does not need a decision, and the secretary will often *record* such a matter in the minutes by writing "The committee *noted with appreciation* (or: *with regret, with pleasure, with thanks, with concern*, etc.) that . . .".

When an ad hoc committee has finished the special work it was set up to do, the chairman (or a meeting of the main committee) may formally *dissolve the committee*, and it then ceases to exist.

A committee may decide to *reverse* one of its decisions; to do this it must pass a special motion to *rescind* the previous one. Notice that the *rescision* of a motion requires another motion at a later meeting.

If a member or his family would benefit by a certain decision of a committee, he should not participate in the debate or the voting on it. Instead he should *declare his (personal) interest*, and either leave the room or remain silent (according to the chairman's ruling) until after the vote. But, if a member thinks his words or his conduct or his attitude have been misunderstood, he can ask permission to *make a personal explanation*.

A committee may be permitted to *fill a vacant seat* by *nominating* someone who would be *eligible* for election in ordinary circumstances. There may be several *nominees* and then the committee votes to *accept or reject the various nominations* in the usual way. No-one should be elected who would be ineligible at an ordinary election. A committee may also sometimes be given power to *co-opt* an extra member; the *co-option* of a member is done by *majority vote* following the usual procedure and a *co-opted member* usually has full voting rights. The conditions for *eligibility* and *ineligibility* should be stated clearly in the committee's constitution or terms of reference.

A committee may appoint another committee from among its own members for some special purpose; this smaller group is called a *sub-committee*. A sub-committee whose members are specially selected like this is often

called a *select committee*, especially when it is appointed by Parliament. A committee that is never dissolved (though its members may be changed) is called a *standing committee* (e.g. the health committee or the finance committee of a council). When a committee wants a sub-committee to consider some matter, it "*refers*" the matter to the sub-committee. This *referral* of a matter is also done by passing a *formal motion*. A sub-committee usually only has powers to make *recommendations*; it is the *full committee* that makes the final decision. When the full committee decides in accordance with the recommendations of the sub-committee, it is said to *adopt* the sub-committee's report.

While the chairman is introducing or explaining an item of business other members must not interrupt him. When he is finished and the time comes for others to speak, we say that he *throws the question open*. He may say "I now throw the question open" or "The question is now open for discussion".

Sometimes a question is asked in a committee meeting and the answer (perhaps because it is unsatisfactory or incomplete or suggests some other important and relevant point) calls forth another question; this is known as a *supplementary question*. (In Parliament, written notice must be given before certain kinds of question can be asked, but a supplementary question can usually be asked *without notice*.)

Under certain circumstances office bearers (of a co-operative society, for example) may be permitted to take action without consulting the committee. In all such cases they should make a report to the committee afterwards, and if the committee is satisfied with their action it will *ratify* their decision. This *ratification* of action that has already been taken is often very important.

If a meeting is called, but cannot be held at the time announced, it is said to be postponed. (Note the difference between *postponing* a meeting and *adjourning* it after it has begun.)

The English word "honorary", which is often used in committees, means "without payment", and we speak of an Honorary Treasurer, or of honorary work, an honorary post, etc.

Finally, committees should *word* their resolutions with great care; important legal matters often depend upon the exact *wording* that is used.



